

## MAZOEZO WAKATI WA LIKIZO

### FORM II -2021

#### ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

1. (a) Ni yapi maandalizi ya kiimani waliyoyapata maswahaba wa mtume SAW wakiwa makkah kabla ya kuhamia Yathrib ?  
(b) Ni lini mtume SAW alifika Quba, na alipokelewa au kujipomzisha nyumbani kwa nani ?  
(c) Ni lini ulijengwa msikiti wa Quba ambao umesifiwa sana katika Qurani (9:108) ?  
(d) Yathrib ilianza kuitwa Madina Al-munawara wakati gani, Aliempokea na kukaa na mtume Muhammad SAW Madina nyumbani kwake anaitwa.....
2. Taja taasisi alizozitumia mtume SAW katika kuusimamisha na kuanzisha dola ya kiislamu madina.
3. Elezea kwa kifupi kwamba ni kweli Uislamu unatambuwa uwepo wa KATIBA, kwa kufafanua:  
(a) Nani mwanzilishi wa katiba.  
(b) Ni kwa nini alianzisha katiba kama ni kweli ?  
(c) Je katiba hiyo ni kama tuliyonayo sisi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ?  
(d) Kama mtume amewahi kuandika katiba ya kuongoza nchi Elezea ilikuwaje muundo wake.
4. (a) Nini maana ya dola kwa mtazamo wa kisekula (Fafanua na muundo wake)  
(b) Uislamu unasemaje kuhusu dola, Je ni kweli inaanzishwa na wanadamu ? Toa ushahidi.  
(c) Ni zipi tofauti kati ya hoja/nadharia za kuibuka kwa dola mbalimbali kwa mtazamo wa kisekula na kiislamu ?
5. (a) Nani mtawala katika dola ya kiislamu ?  
(b) Taja misingi mikuu mitatu ya utawala katika dola ya kiislamu.  
(c) Lengo la dola ya kiislamu mahali popote ni kudumisha mambo manne, Yataje kwa ufupi.
6. Onesha udhaifu wa mifumo ya utawala wa dola kwa kutumia.  
(a) Demokrasia ya vyama vingi au kimoja.  
(b) Ukomunisti.  
(c) Ufashisti.
7. Elezea namna KADHI (Majaji) wanavyoteuliwa kisha kwa ufupi toa utaratibu wa mahakama katika yafuatayo:  
(a) Uwepo wa wale wanaoshtakiana  
(b) Haki au wajibu wa Mshitaki  
(c) Wajibu au haki ya mshitakiwa  
(d) Kazi au wajibu wa Kadhi kwa Mshitakiwa.
8. Taja na kufafanua mambo makuu manne ya kuzingatia katika kupata ufafanuzi wa matatizo katika dola ya kiislamu au kuendesha dola ya kiislamu.
9. Eleza kwa kifupi mgawanyo wa Serikali ulivyokua katika dola aliyoiongoza mtume SAW
10. Elezea sifa za kiongozi yeyote wa dola ya kiislamu, mipaka ya kumtii, Namna ya kutatua matatizo ya kidini kwa SHURA pia upi umuhimu wa SHURAA.